

Sala sita za mtume zinazosomwa  
kila wiki katika Ijtimai ya  
kuhamasisha sunna ya Dawat-e-Islami

## SALA SITA ZA MTUME

### 1 Sala ya Mtume kwa ajili ya usiku wa Ijumaa

اللَّهُمَّ صَلِّ وَسَلِّمْ وَبَارِكْ عَلَى سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ  
النَّبِيِّ الْأُمِّيِّ الْحَبِيبِ الْعَالِي الْقَدْرِ الْعَظِيمِ  
الْجَاهِ وَعَلَى آلِهِ وَصَحْبِهِ وَسَلِّمْ

Wanazuoni wa kiislamu wamesema kwamba mtu anaesoma sala hii ya Mtume angalau mara moja katika usiku wa Ijumaa (usiku wa Alkhamis kuamkia Ijumaa), atapata baraka za Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ katika mauti yake na hata akifika kaburini mwake atamuona Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ ndie anaamlaza kaburini kwa mikono yake yenye rehema.

(Afzal-us-Salawat 'ala Sayyid-is-Sadaat, uk. 151)

## 2 Milango 70 ya rehema

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى سَيِّدِنَا وَمَوْلَانَا  
مُحَمَّدٍ وَعَلَىٰ آلِهِ وَسَلَّمَ

Sayyiduna Anas رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ amepokea kwamba Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, 'Kama mtu ataisoma sala hii ya Mtume wakati amesimama atasamehewa dhambi zake kabla hajakaa, akiisoma akiwa amekaa atasamehewa kabla ya kusimama.' (Ibid, uk. 65)

## 3 Madhambi yake yatafutika

صَلَّى اللهُ عَلَى مُحَمَّدٍ

Mtu anaemsalia Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kwa sala hii, milango 70 ya rehema itafunguliwa kwa ajili yake. (Al-Qaul-ul-Badi', uk. 277)

4

Ujira wa 600,000  
kwa sala Ya Mtume

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ  
عَدَدَ مَا فِي عِلْمِ اللَّهِ صَلَاةً دَائِمَةً  
بِذَوَامٍ مُلْكِ اللَّهِ

Imam Ahmad Sawi عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْهَادِي amepokea kutoka kwa moja ya wacha mungu kwamba yoyote atakaemsalia Mtume صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kwa sala hii mara moja, atapata ujira wa kusoma sala za Mtume mara laki sita.

(Afzal-us-Salawat 'ala Sayyid-is-Sadaat, uk. 149)

5

Ukaribu Kwa mtume  
mtukufu ﷺ

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ  
كَمَا تُحِبُّ وَتَرْضَى لَهُ

Siku moja alikuja mtu kwa Mtume ﷺ na Mtume ﷺ akamruhusu akae baina yake na Sayyiduna Abu Bakar Siddik رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُ.

Masahaba wakapatwa na mshangao juu ya yule mtu kwa heshima aliyopewa. Baadae yule mtu alipoondoka, Mtume ﷺ akasema: 'Yule mtu akinisalia basi hunisalia kwa sala hii'

(Al-Qaul-ul-Badi', uk. 125)

## 6 Matendo mema kwa siku 1000

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَأَنْزِلْهُ  
الْمَقْعَدَ الْمُقَرَّبَ عِنْدَكَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ

Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, 'Maombezi yangu yatakua lazima juu yangu kwa atakaenisalia namna hiyo.'

(Al-Mu'jam-ul-Kabeer, juz. 5, uk. 25, Hadees 4480)

## Dua Mbili

### 1 Matendo mema kwa siku 1000

جَزَى اللهُ عَنَّا مُحَمَّدًا مَا هُوَ آهِلُهُ

Sayyiduna Abbas رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ amesimulia kwamba Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, 'Kwa anaesoma sala hii ya mtume, malaika sabini watamuandikia ujira wa matendo mema kwa masiku elfu. (Majma'-uz-Zawaid, juz.10, uk.254, Hadees 17305)

2

## Njia rahisi ya kuutumia usiku kwenye ibada

Ikiwa mtu atasoma dua ifuatayo kila usiku, atakuwa kama aliepata Layla tul Qadr.

لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ الْحَلِيمُ الْكَرِيمُ، سُبْحَانَ اللَّهِ  
رَبِّ السَّمَوَاتِ السَّبْعِ وَرَبِّ الْعَرْشِ الْعَظِيمِ

Kwa hiyo dua hiyo isomwe kila usiku kama ifuatavyo:

**Majlis-e-Tarajim (Translation Department)**

Faizan-e-Madinah Mahallah Saudagran, Purani  
Sabzi Mandi, Karachi

UAN: ☎ +92-21-111-25-26-92 – Ext. 7213

Email: ✉ [translation@dawateislami.net](mailto:translation@dawateislami.net)